REPUBLIC OF KENYA

PENAL REFORM INTERNATIONAL

Hukumu za huduma kwa jamii na probesheni kwa wanawake

Mafunzo na mapendekezo kutokana na utafiti nchini Kenya

Soma taarifa nzima ya utafiti*

Angalia makala fupi kwenye filamu

Inapatikana kwenye tovuti:
www.penalreform.org





Utangulizi

Wanawake na wasichana ni kundi dogo sana kwenye mfumo wa mahakama, ambalo linafikia kati ya asilimia mbili hadi tisa ya idadi ya wanawake walio gerezani nchini. Kwa hali hiyo, wanajikuta kwenye mfumo wa mahakama za uhalifu ambazo zinalenga kushughulikia kundi kubwa la idadi ya wafungwa wa kiume bila kuzingatia mahitaji ya wahalifu wa kike na mazingira yao. Hali hii ilidhihirika mwaka 2010 wakati jumuiya ya kimataifa ziliporidhia Kanuni za Umoja wa Mataifa katika kuboresha hali za wanawakewaliofungwa magerezani na hatua za uangalizi wa wanawake wahalifu wanaotumikia kifungo cha nje au kanuni za Bangkok ambazo zinaorodhesha mambo ya kufanya ili kuhakikisha mambo nyeti[1] ya kijinsia yanapewa uzito ndani ya magereza na kwenye kifungo cha nje au vikwazo.

Sheria za Bangkok zinasisitiza wazi kuanzishwa na kutumika njia mbadala zinazozingatia kijinsia kwa kifungo cha nje wakati wa kuzuiwa kabla na baadaya kuhukumiwa na kufungwa. Hali hii ni kutokana na kutambua ukweli kwamba watuhumiwa na wahalifu wanawake si tishio kwa jamii, pia kuwafunga kuna athari kubwa kwenye urekebishwaji wao binafsi na kwa maisha ya watoto wao.

Kwa upande mwegine, hatua za vikwazo kwakifungo cha nje ambavyo vinazingatia mahitaji bainifu ya wanawake zinawawezesha wanawake kutekeleza majukumu yao ya ulezi wakati huo huo wakitumikia hukumu zao. Utaratibu huu unaweza kuwa njia yenye ufanisi zaidi katika kukabiliana na sababu za msingi za kufanya makosa badala ya kuwa ndani ya jela. Ni jambo la muhimu kuweka mkazokwamba kuwatendea wafungwa wa kike tofauti na wenzao wa kiume kimsingi si uonevu wala ubaguzi, kinyume chake ni haki. Wahalifu wa kike wana mahitaji tofauti kabisa ambayo yanatakiwa kubainishwa na kushughulikiwa ili kupata matendo yenye usawa.

Katika utekelezaji wa Mradi wa Mageuzi ya adhabu ulioendeshwa na Penal Reform International ikishirikiana na Kenya Probation na Aftercare Service kuhusu hukumu za huduma kwa jamii na probesheni kwa wanawake nchini Kenya, uliofadhiliwana Thailand Institute of Justice, utafiti ulifanyika mwaka 2016[2] ili kuchunguza mfumo uliopo na uzoefu wa wanawake wanaotumikia hukumu kwa vikwazo vya huduma za jamii.

Popote walipo, wahalifu wakike wanakabiliwa namatatizo yale yale kama vile kubaguliwa, unyanyapaa, kukumbana na kiwango kikubwa cha ukatili, na umaskini. Hivyo basi, kutokana na utafiti wa hali ilivyo Kenya, tunapata mafundisho na mapendekezo kuhusu njia za kushughulia vikwazo vya kijamii kijinsia ambavyo vitalingana na nchi nyingine. Haya maelezo mafupi yanatokana na utafiti uliofanywa na Penal Reform International na tafiti nyingine zinazohusu wanawake walio kwenye mfumo wa mahakama za jinai.[3]

* Inapatikana kwa Kiingereza.

Makosa na utaratibu wa uendeshaji wa kesi

Matokeo ya utafiti na mapendekezo

1. Makosa mengine yanaathiri zaidi wanawake kuliko wanaume

Makosa ya uhalifu yanaweza kuonekana sawa kwa jinsia zote, lakini kulingana na hali halisi makosa mengine yanasababisha adhabu kali kupita kiasi kwa wanawake pekee. Kwa mfano, tafiti zinaonyesha kuwa katika baadhi ya mikoa asilimia kubwa ya wanawake wahalifu kwa makosa yanayohusu madawa ya kulevya wanapewa hukumuzinazobaguakijinsia katika 'kupigana vita dhidi ya madawa ya kulevya'. Katika baadhi ya nchi wanawake na wasichana wanahukumiwa kwa 'utoro' baada ya kuondoka nyumbani kwao bila ruhusa. Mara nyingi wanakimbia ukatili wanaofanyiwa na ndugu zao ndani ya familia. Kwa ujumla wanawake ndio wanahukumiwa zaidi kwa makosa ya ukahaba zaidi kuliko wanaume.

> "...Makosa mengi ya wahalifu wanawake hufanyika wakati wanajitafutia kipato na wala sio kutokana na tabia za kiuhalifu."
>
> Afisa wa Majaribio, Kenya.

Makosa kwa wanawake yanahusishwa kwa karibu sana na uchumi na kukosa kunufaika kijamii. Utafiti uliohusu wanawake wanaotumikia hukumu kwa kufanya huduma kwa jamii au kuwa kwenye majaribio nchini Kenya ulibainisha kuwa kuna tofauti ya utoaji hukumu kwa wanawake ukilinganisha na wanaume ambao wana makosa yanayohusu kujikimu kiuchumi na kusaidia familia zao.Makosa hayo yanahusu shughuli za kujipatia kipato kwa kutengeneza pombe za kienyeji na kuuza vinywaji vya kilevi bila leseni na ukusanyaji wa kuni kutoka kwenye misitu kwa ajili ya kupikia (makosa chini ya sheria ya uhifadhi wa wanyama pori). Hukumu za makosa madogo zina athari kubwasana kwa wanawake na mara nyingi huendeleza umasikini kwao na familia zao. Hata jamii haifaidiki chochote kwa kuwafunga wanawake jela kwa makosa madogomadogo.

> "Huwezi kumhukumu mwanamke ambaye amepatikana msituni akinatafuta kuni za kupikia kwa adhabu sawa na mtu ambaye anakutwa akikata miti kwa minajili ya kupata magogo. Mwanamke huyu anafanya hivyo ili ahudumie familia yake."
>
> Micha Powen, Katibu Mkuu, Huduma za Marekebisho ya Tabia kwa wafungwa nchini Kenya.[4]

→ Hatua ya kufuta makosa madogo ni lazima itambuliwe kuwa ni jitihada za kupunguza msongamano kwenye mfumo wa mahakama na kuhakikisha haki na usawa katika vikwazo. **(Tokyo Rule 2.7, Bangkok Rules 57-58)**

2. Utaratibu wa uzuizi kabla ya kusikizwa kesi kunatumika zaidi kupita kiasi kwa wanawake watuhumiwa

Sheria zote za Umoja wa Mataifa kuhusu sheria za kifungo cha nje (Sheria za Tokyo) pamojana sheria za Bangkok zinahimiza mfumo wa hukumu kutoa fursa nyingi mbadala uzuizi kablaya hukumu. Watuhumiwa wa kike watanufaika zaidi na njia hizi mbadala kwa sababu wao ndio huwa wanahukumiwa kwa makosa madogo na yasiyotumia nguvu na wao si tishio kwa jamii. Uzuizi kabla ya kusikizwa kesi hatakama ni kwa kipindi kifupi kunaweza kuwa na athari kubwa na madhara makubwa kwa watoto na familia zao.

> "Niliposhikwa nilipoteza biashara yangu."
>
> Mhalifu wa kike, Kenya.

Hata hivyo, wanawake katika nchi nyingi wanaishia kuzuiliwa kwa sababu fursa za kawaida za adhabu zisizo za kifungo cha jela kama vile kulipa faini na kupata dhamana hazizingatii jinsia na haziwafai wanawake. Kwa mfano, kwenda kituo cha polisi kama sehemu ya masharti ya dhamana kunaweza kuhitilafiana na majukumu ya wanawake ya utunzaji wa familia. Wanawake wanaweza kukosa dhamana kama hawamiliki mali (kisheria au kwa sababu za kiuchumi), na pia kiwango cha dhamana wakati wote ni zaidi ya uwezo wao.

Hali hii inafaa zaidi Kenya ambapo asiliamia (87) ya wanawake waliohojiwa wakati wa utafiti walijibu kuwa walizuiliwa kabla ya kuhukumiwa. Kufuatia utendaji wao na nidhamu wakati wa huduma kwa jamii au amri ya Majaribio (rekodi zinaonyesha kuwa ni chini ya asilimia tano pekee za kesi zilikuwa na alama 'waliotoroka/jificha'au 'hazikuridhisha/hawakumaliza vizuri') ni ishara kubwa kwamba wangeweza kuhudhuria mahakamani bila hata ya kuwaweka kizuizini. Wanawake walioshiriki kwenye utafiti walieleza kuwa kuzuiliwa kabla ya hukumu kuliwaharibia shughuli zao za kujitafutia kipato pia kulileta athari kwa uangalizi wa watoto. Watoto wanaolelewa na mama pekee wakati mwingine huachwa bila usimamizi wa mtu mzima na wanawakewengine walizuiliwa na watoto wachanga kwa hali ya kutatanisha.

> "Mjukuu wangu wa kike ambaye ninamtunza alipata ujauzito nilipokuwa kizuizini na kwa sasa ameacha shule. Mimi ndiye."
>
> Wahalifuwa kike Kenya.

Kati ya wanawake waliopata dhamana wengi wao hawakuweza kukidhi masharti ya dhamana yaliyowekwa. Ni asilimia sita tu ndio walipata mawakili wa kuwasaidia bila hivyo wasingeweza kupata dhamana.

Wakati mwingine, ucheleweshaji wa kuwasilisha taarifa/ripoti kutoka kwa Afisa wa marekebisho/probesheni kabla ya hukumu kulisababisha kuzuiliwa kwa muda mrefu kusuburi kusikilizwa shauri.

➔ Inafaa wanawake wapate msaada wa mawakili kwenye mahakama wakati wote wa kusikiliza kwa kesi, na hasa wakati wakusikilizwa kwa shaurilinalohusu kupata dhamana ili kupunguza kiwango cha idadi ya watuhumiwa kuzuiliwa kabla ya hukumu. Pale ambapo haiwezekani kumpata wakili wa kulipiwa na serikali, hakimu watalazimika wao wenyewe wafanye uchunguzi wakati wa kusikiliza shauri la dhamana. **(UN Principles and Guidelines on Access to Legal Aid in Criminal Justice Systems, Guideline 9)**

➔ Maafisa wa mahakama inafaa watumie njia mbadalakwa mtuhumiwa kuwa nje ya rumandekwa kuzingatia jinsia kabla ya kusikilizwa kesi zao. **(Bangkok Rules 57-58)**

3. Umuhimu wa ripoti kabla ya hukumu

Muongozo wa kutoa hukumu rasmi na isiyo rasmi na ripoti kabla ya hukumu (taarifa ya uchunguzi za kijamii) na vigezo vinavyotumiwa na huduma ya probesheni pamoja na Mahakama kwa kawaida huwa zinazingatia usawa wa kijinsia na ziwe na uwezekano wa kufanyiwa marekebisho ya kufaa ili mahakama iweze kukumbuka hali jinsi ilivyo ambazo zinaweza kuzingatia mazingira au tabia za kijinsia. Kwa mfano, kuwa mlezi wa pekee wa watoto au ndiye anayetegemewa na familia., au kuwa na mahitaji makubwa ya afya ya kiakili, ni baadhi ya mambo binafsi yanayoweza kupunguza makali ya miongozo ya kutoa hukumu.

Sheria za Bangkokzinawalazimisha maafisa wa mahakama (kama vile mahakimu na majaji) kutumia busara zao wanapotoa hukumu kwa wahalifu wa kike waweze kuzingatia mambo ambayo yanaweza kupunguza ukali wa adhabu pamoja na maelezo ya taarifa kabla ya hukumu.

Ripoti hizi ni muhimu zaidi kwa sababu zinafichua mazingira ya kipekee ya kijinsia kwa wahalifu wanawake na kusaidia kuamua aina ya hukumu inayostahili katika mazingira husika.

Nchini Kenya, maafisa wa mahakama walieleza kwamba mara nyingi huomba ripoti ya kabla ya kutoa hukumu kwa wanawake ili iwaongoze wakati wa kutoa hukumu. Hata hivyo, maafisa wa majaribio huwa hawatoi taarifa kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali kama vile ukosefu wa fedha, ripoti hizo kuwa na ubora unaotofautiana, na huwa hazina ukweli mara zote, zinaonyesha upendeleo, na ubaguzi kama inavyoelezwa katika Kanuni ya sita ya Tokyo.[6] Zaidi ya hayo, ni muhimu kuwepo na chombo chenye kiwango kinachokubalika katika kukusanya taarifa na kuwasilisha taarifa kabla ya hukumu, bila chombo hicho uzingatiaji wa mambo ya kijinsia yategemea busara ya afisa wa probesheni.

Katika mazingira mengi, na wala si Kenya tu, kuna umuhimu wa kuimarisha ubora wa taarifa kwa maafisa wa mahakama ili hukumu ziendane na Sheria za Bangkok.

➔ Taarifa ya kabla ya hukumu au ripoti za kijamii zinapaswa kuwa tayari/kupatikana kwa maafisa wa mahakama wakati wa kutoa hukumu, na lazima ziwe na taafrifa kuhusu majukumu ya wanawake, historia yo yote ya dhuluma, mahitaji ya afya ya kiakili na utegemeaji wa madawa. **(Bangkok Rule 61)**

➔ Wale wanaoajibika kutayarisha hizi ripoti lazima wawena vifaa vya kutosha, muongozo na mafunzo ili uchunguzi wao na ripoti za kabla ya hukumu ziwe za kutofautisha kijinsia na zitayarishwe kimaadili na kitaalamu. Maswala muhimu lazima zinakiliwe kwa uthabiti badala ya kuachiwa afisa wa probesheni kutumiabusara yake. **(Tokyo Rule 7.1)**

Maelezo ya wanawake wanaotumikia vifungo vya nje au huduma kwajamii nchini Kenya

Historia na tabia za wanawake wahalifu nchini Kenya ni sawa kwa namna nyingi na historia na tabia za wanawake wahalifu wa nchi nyingine.*

Mahojiano inaonyesha kwamba wengi wa wanawake wanao tumikia kifungo cha huduma kwa jamii au cha nje (probesheni) nchini Kenya walikuwa:

- **mama wenye watoto wadogo:** robo tatu walikuwa na watoto waliochini ya miaka 18.
- **wenye elimu ya chini:** asilimia 21 tu ndio walipata elimu ya sekondari na hakuna hata mmoja mwenye elimu ya chuo kikuu.
- **wenye kipato cha chini:** wengi wao walifanya kazi kwenye sekta isiyo rasmi kilimo na kazi za ndani kama vile ususi, kuuza bidhaaza nyumbani na vyakula/vinywaji.
- **walio hukumiwa kwa makosa madogona yasiyo ya kutumia nguvu:** kwa mfano, asilimia 36 ya wanawake walihukumiwa kwa kuuza pombe bila leseni na kwa makosa madogo kama vile kukusanya kuni ndani ya msitu na kushindwa kutojenga choo.
- **kukosa ili kupata pesa:** asilimia 67 walisema walitenda makosa ili wapate pesa ya kusaidia familia zao.
- **hawana uwezo wa kupata wakili:** asilimia sita tu ndio waliweza kupata mwanasheria wa kuwawakilisha wakati wa kesi inapoendelea.
- **manusura ya dhuluma:** asilimia 33 walikiri kutendewa ukatili katika familia angalau wakati mmoja katika maisha yao.[5]
- **hali mbaya ya kiafya:** wanawake wengi waliohojiwa walikuwa na Virusi auwanaishi na/wame ambukizwa UKIMWI.
- **hakuna ujuzi/bila ujuzi:** wanawake wengi waliohojiwa walikuwa hawajui kusoma na walikuwa na ujuzi mdogo.

* Soma utafiti PRI ya: '*Who are women prisoners?*' Kwa taairfa zaidizinapatikana: www.penalreform.org.

Kuelekea hukumu zinazo zingatia jinsia katika jamii

Matokeo ya utafiti

Sheria za Bangkok zinasisitiza kuanzisha na kutumika kwa njia mbadala kabla ya kuhukumiwa zenye kuzingatia jinsia ili kutoa nafasi ya kutumikia hukumu kwa kifungo cha jela (na kupata dhamana kabla ya kuhukumiwa). Njia hizi zinazingatia 'historia ya uonevu kwa wanawake wengi wahalifu na majukumu yao ya kutunza watoto'. **(Rule 57)**

Hukumu zinatumika ndani ya jamii kuepuka gharama kubwa ja kijamii na za kiuchumi za jela na pia utaratibu huu umedhihirika kuwa na ufanisi mkubwa kuliko wa kifungoni katika kudhibiti kurudia kutenda makosam hasa kwa wanawake wanaohukumiwa kwa makosa madogo, makosa, yasiokuwa ya kikatili. Hata hivyo, hukumu za kifungo cha nje zinapangwa kulingana na mahitaji na mazingira ya wahalifu wa kiume na kusahau uhalisia wa tofauti za maisha ya wanawake. Kwa mfano, umaskini uliokithiri wa wanawake wahalifu na utegemezi wao kwenye familia ya mwanaume ina maana kunasababisha washindwe kulipa faini ambayo hutolewa kama njia mbadala ya kukwepa kwenda jela kwa makosa madogo. Ni kutokana na mazingira hayo, wanaishia kupewa adhabu kali zaidi.

Mahojiano na wanawake nchini Kenya yalionyesha namna wanavyofurahia utaratibu wa kutumikia hukumu nje ya Jela kwa Amri ya Majaribio[7] na Amri ya Huduma za Jamii[8] (CSOs) badala ya kutumikia kifungo gerezani, si haba kwa sababu inamaanisha wataweza kutimiza majukumu ya familia kama vile kuangalia watoto na jamaa wengine wa familia. Hii ni pamoja na kuendelea na shughuli za kuzalisha kipato ambazo kitawasaidia wanafamilia.

Hata hivyo, kulikuwa na changamoto nyingi zilizotokana na vikwazo vya jamii. Kutokana na mahojiano ilibainika baadhi ya matatizo ya kuridhia kwa sababu mgongano wa majukumu binafsi ya kifamilia, madhalani, kuangalia watoto, ujauzito, kuolewa tena na kuhamia mahali pengine au kuhudhuria misiba (pale ambapo mahudhurio yanatalajiwa kwa siku kadhaa itahusisha uchangiaji na kushiriki katika shughuli za kupika, etc.). Baadhi ya wanawake walisema kuwa waliamua kuhamia eneo linguine kukimbia kipigo kutoka kwa waume zao. Orodha ifuatayo inatoa maelezo mafupi ya changamoto kwa wananwake wanaotumikia hukumu ya Majaribisho nchini Kenya ambayo inaaminika inastahi nadhani inaweza.

- Mahakama inapendelea kutoa Amri ya Majaribio na CSO badala ya faini kwa sababu baadhi ya sheria zinatamka kiwango cha chini cha faini ambacho kwa upande wa wanawake ni kikubwa mno kiasi cha kusababisha kwenda jela kwa kushindwa kulipa faini.
- Idadi kubwa ya wanawake ambao wanatumikia Amri ya Majaribio nay a kufanya kazi za huduma ya jamii walisema kuwa walijitahidi sana kuweka akiba ya fedha kulipia usafiri wa kwenda office ya Majaribio na cha huduma za Jamii au kituo cha 'kazi'. Hili sio jambo la kushangaza kwa sababu umaskini ulikuw chanzo cha makosa yao.
- Kutokana na kuwepo kwa vituo vichache vya 'kazi' vinavyofaa kwa wanawake wanaotumikia hukumu kwa kufanya kazi za huduma za jamii wale wanaopangwa wakuta vituo vipo mbali na wanapoishi. Muda wanaotumia kusafiri kutoka kwenye vituo hivi unaathiri majukumu yao ya kutunza familia na kupunga furas zao za kupata kazi za vibarua akabla na baada ya kutoka vituoni kwao kwa siku. Hata hivyo, kwa wanawake ambao wanapangiwa vituo ambavyo viko karibu na muda wa kazi unapangwa kiasi cha kuruhusu siku za mapumziko, waliweza kujikimu kifedha na kufanya majukumu ya wakati huohuo wanatumikia hukumu zao.
- Jumla ya masaa ya katika ratiba ya kazi ya Huduma kwa Jamii yaliathiri wanawake wengi kwa upande wa majukumu yao kulea na kujipatia kipato. Kutokana na changamoto za ubali wa kwenda kituoni kufanya kazi, kulazimika kufanya kazi kwa masaa mawili kila siku kwa siku tano ilisababisha kupoteza masaa muhimu ya asubuhi ambako kazi nyingi za vibarua hupatikana. Ilielezwa kuwa, kwa mfano: '*Mama mjane mwenye motto mgonjwa alienda kuomba msaada kwenye kituo chake kwa sababu isingekuwa rahisikuttibiwa kwa KES 50 [0.50] ambazo zilihitajika zahanati. Mama mjane hakuwa na fedha kwa kuwa hakuwa amefanya kibarua siku hiyo.'*

Mapendekezo ya huduma za jamii na majaribio kwa wanawake

Baadhi ya mapendekezo yaliibuka kutokana na utafiti wa PRI's nchini Kenya katika kuangalia namna ambavyo wadau mbalimbali wa mfumo wa mahakama ya jinai wanaweza kusaidia kutoa nafasi ya kutumia hukumu za kifungo cha nje – kwa kufanya huduma kwa jamii na Majaribio kuwa na utaratibu ambao unazingatia jinsia.

→ Uwezo na Ufahamu kuhusu maswala ya jinsia – mambo mahususi miongoni mwa wadau wa mahakama ya jinai

Wadau wote wahusika katika mfumo wa mahakama ya jinai wanatakiwa kutambua viashiria na mahitaji ya wanawake wahalifu na pia ni muhimu wapate mafunzo namna ya kutumia sheria za Bangkokna zaTokyo. Jitihada za mafunzo ni lazima zihusishe wadau wote wanaostahili hawa ni pamoja na maafisa wa probesheni, majaji, mahakimu, pamoja na maafisa wasimamizi. Uwasilishaji kwa kuwachanganya makundi ya wadau umekuwa na mafanikio sanal.[9]

Katika kubainisha na kushughulikia mambo yanayosababisha uhalifu, inabidi serikali itenge fedha za kufanyia uchambuzi wa takwimu na tafiti kwa shirikia na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayoshughulikia wanawake wahalifu. Katika: kukusanya taarifa kwenye maswala yanayojitokeza kwa wingi na kusababisha wanawake kuingia kwenye mfumo wa mahakama ya uhalifu na kujua kiwango ya kurithia amri ya huduma kwa jamii na kuiarifu ratiba zinazo saidia utekelezaji vikwazo ndani ya jamii. PRI's 'Community Service Measurement Tracker' ni raslimali muhimu ya kusaidia kuboresha ukusanyaji wa takwimu.[10]

Utekeleza mzuri nchini Kenya: Jitihada za uwezesha kiuchumi

Uwezo Initiative katika eneo la Kibera wanawapa wanawake wahalifu ujuzi wa msingi wa kufanya ujasiliamali na kuwasaidia kuanzisha biashara ndogo ndogo kama vile kuuza mitumba na vibanda vya kuuza vyakula. Baadhi ya wanawake wameeleza kuwa kutokana na mpango huo walifanikiwa kuwa na kipato na wamehamasika kuendelea. Kuna baadhi ya changamoto zilijitokeza kama vile kuendeleza biashara wakati wa hali 'ngumu za maisha' na wakati wanahitaji mikopo ili kuwekeza tena kwenye biashara zao. Hata hivyo, wanawake waliohojiwa walibainisha kuwa wamedhamiria kutokufanya makosa tena kwa sababu kwa sasa mahitaji yao ya fedha yametika.

Mnufaika mmoja wa mfuko huu alieleza: *'Sasa nina duka; Uwezo wamenisaidia fedha za kuanzishia duka na ninaendelea vizuri. Kaka yangu hunisaidia kuuza dukani ninapo hitajika kwenda kupiga ripoti kwenye ofisi ya probesheni kila mwezi.'*

Maafisa wa Majaribio lazima watiwe moyo kuhifadhi kumbukumbu za uzoefu wao wanapokuwa na wanawake wahalifu nakujifunza kutoka kila mmoja wao na kubaini mbinu nzuri za utendaji.

→ Zifaazo za kushughulikia changamoto za wanawake wanaotumikia kifungo cha huduma kwa jamii

Maswala ya kufaa yastahili kuzingatiwa wakati wa kupanga huduma kwa jamii. Inafaa kutengewa maeneo ya huduma ambayo yapo karibu sana iwezekanavyo na nyumbani kwa mkosaji ili kumpunguzia gharama za usafiri na muda wa kusafiri. Muda wakazi upangwe ili uendane na majukumu ya kifamilia. Masaa ya kazi ya tengenezwe ili yaambatane na majukumu ya kifamilia. Upangaji wa maeneo ya kazi lazima usimamiwe namaafisa wanaofahamu mazingira binafisi ya mwanamke mhalifu anayewasimamia. Maeneo ya kazi yasimamiwe na maafisa wanaofahamu hali ya mwanamke mhalifu aliye chini yao.

Zaidi ya hayo, upangaji kazi inapasa uzingatie ujuzi, afya kwa ujumla na uwezo wa mwili wa mwanamke. Inabidi wawekwe kwenye hali ambayo inazingatia utamaduni na tofauti za wenyeji, wakati huohuo wakiepuka ubaguzi kazi wa kijinsia (kwa mfano, wasipangiwe kazi zinazodhaniwa ni za wanawake tu kama vile usafi na kupika).

→ Usalama kwa wanawake wanapokuwa wanatumikia Kifungo cha huduma kwa jamii

Wengi wa wanawake waliohojiwa nchini Kenya hawakuzungumzia visa au malalamiko kuhusu usalama wa kibinafsi wakati wa kutumikia kifungo cha huduma kwa jamii. Hata hivyo ukatili dhidi ya wanawake, pamoja na dhuluma za kimapenzi, inajulikana kuripotiwa kwa uchache sana.[11]

Utafiti umeonyesha kwamba kuna manufaa ya programu za kuwahudumia wanawake tu ambayo imeangaziwa kwa sheria za Bangkok. Zana nyingine ya kulinda usalama wa wanawake wakati wanatumikia kifungo cha nje ni utaratibu wa kuwasilisha malalamiko ambazo zitawezesha wanawake kuwasiliana na mtu wanayemwamini kwa njia ya siri, hasa kwenye maswala ya kuhangaishwa kimapenzi, ukatili na unyonyaji. Inaweza kuwa ni jambo la muhimu kutotaja jina la mlalamikaji pia mwanamke huyo ni lazima ahakikishiwe kuwa malalamiko yoyote hayatatafsiriwa kuwa ni dalili za kutotaka kutumikia adhabu ya hukumu.

> "Afisa Utawala wa polisi alikuwa akininyanyasa kimapenzi. Nilipinga ombi lake na kutoa taarifa kwa kwa afisi ya probesheni hali ambayo ilisababisha ahamishwe."
>
> Mwanamke anayetumikia kifungo cha Huduma kwa Jamii nchini Kenya.

Ijapokuwa wanawake wa Kenya waliohojiwa hawakuona umuhimu wa kusimamiwa na afisa wa probesheni wa kike, kwa upande mwingine uwepo wa mwanamke ingefaa kwa ajili ya kuwalinda wanawake.

Wanawake wahalifu hawapaswi kusimamiwa na mtu ambaye alihusika kwa kukamatwa kwake.

→ Kujenga ujuzi na programu nyingine saidizi

Mambo kama kiwango kidogo cha kujiamini na ukosefu wa ujuzi wa maisha, kama vile namna ya kusimamia majukumu kama mzazi au msongo wa mahusiano, yamepatikana kuwa na umuhimu sana kwa wanawakewahalifupamoja na kuongeza kwa matatizo ya afya yakiakili. Mambo kama kutokujiamin, ukosefu wa ujuzi wa maisha kama majukmu ya malezi na tatizo la msongo wa mahusiano pamoja na hali ya juu ya matatizo ya kiakili ndiyo yameonekana ni muhimu sana kwa wanawake wakosaji.

Sheria za Bangkok zinatoa mwito kwa sheria za vikwazo vya kifungo cha nje kuingiza mipango ambayo itashughulikia matatizo makuu ya kawaida yanayosababisha wanawake wakutane na mfumo wa hukumu ya uhalifu, kama mafunzo ya ujuzi na ushauri nasaha kwa wanaoathiriwa na ukatili wa ndani ya familia na dhuluma zakimapenzi.[12]

Kwa kuwa umaskini ni chanzo kikuu wa msukumo wa wanawake kufanya makosa kwa namna nyingi, huduma za marekebisho zinazo husu mafunzo ya kazi na uchumi zina umuhimu kwa kushughulikia kiinicha haya/hiki.

> "Ninahitaji pesa za kuanzisha biashara nyingine au ujuzi wa kuniwezesha kuajiriwa, la sivyo sinabudi kurudia kupika pombe."
>
> Mwanamke anayetumikia kifungo kwa jamii, Kenya.

Mbinu shirikishi kwenye jamii husika lazima itumike katika kuunda ratiba ya huduma kwa jamii ili zichangie kwenye mahitaji ya kazi za umma na kuwa na manufaa.

Utekeleza mzuri nchini Kenya: Mipango inayozingatia jinsia kwenye mabweni za probesheni za wasichana

Mabweni ya wasichana ya probesheni 'iliyoko Nakuru', ni moja ya taasisi nne kama hii nchini Kenya ambazo zinazowapa makao wa muda wasichana wakosaji wenye umri kati ya miaka 12 na 22.

Kiwango cha kawaida cha muda wa kutumikia hukumu kwenye hosteli ya majaribio ni mwaka mmoja, lakini katika hali isiyo ya kawaida muda wa kuendelea kutumikia hukumu unaweza kuongezwa kwa kupitia ombi kwa mahakama.

Hosteli inatoa mafunzo ya stadi, ushauri nasaha na huduma za kijamii zinazowalenga wasichana wahalifu. Wasichana waliohojiwa walisifia utaratibu wa hosteli kwa kusema ni tofauti na gerezani, wanaruhusiwa kuja na kuondoka.

Afisa wa probesheni alipohojiwa alisema kadiri wanavyoendelea kwa muda mrefu wameweza kubainisha mahitaji ya wasichana na kurekebisha programu zao ili kushughulikia mahitaji kama vile kuendesha shughuli ambazo zinawawezesha kujistahi, na kujiamini.

Kwa ujumla, ilidhihirika kwamba maafisa wa probesheni wanatambua usawa wa kijinsia. Afisa mmoja wa probesheni alipata mafunzo kutoka PRI juu ya sheria za Umoja wa Mataifa UN Bangkok Rules.

Baadhi ya changamoto zilibainishwa. Pamoja na kuwa familia inasaidia kwenye mchakato wa marekebisho, kwa upande mwengine kuna changamoto ya umbali kutoka nyumbani inayowafanya wazazi washindwe kutembelea wasichana hawa. Pia, pamoja na kuwa wasichana wanaweza kupata elimu rasmi au kujifunza taaluma kama vile ushonaji, kutoa huduma ya kupika hapakuwa na zana au zilizopo ni zimepitwa na wakati na kuna ukosefu wa maangali baada ya kumaliza ili apokelewe na kuwa sehemu ya jamii. Kwa mfano hosteli haina bajeti ya kutoa kiasi kidogo cha mtaji wa kuwasaidia wasichana watumie ujuzi waliopata kama vile kununua cherehani ya kuazishia biashara.

→ Msaada wa Familia Kijamii na kisaikolojia Msaada wa familia na jamiikisaikolojia

Wanawake waliohojiwa nchini Kenya walieleza kwamba msaada wa familia, zikiwa za matendo na fedha, ilikuwa ni sehemu muhimu ya kuwawezesha kutumikia vifungo vyao vyema.

Matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba msaada wa kisaikolojia ya kijamii, kama vile ushauri nasaha, ni hitaji muhimu sana kuzuia kurudia kutenda kosa kwa sababu hasira, msongo wa mawazo na kuishi na mume, mke/mwenzi/mshiriki ambaye ni mnyanyasaji zote ni vizuizi za kumwezesha kutumikia kifungo cha nje cha probesheni au cha huduma kwa jamii na inaweza kuwa sababu ya kurudia kutenda kosa.

Kuna mbinu chache sana za kukabiliana na matatizo ya kiakili nchini Kenya. Msaada wa makundi rika zimeonyesha kuwa za mafanikio Kwa wanawake wahalifu, zikitoa msaada ya namna ya gharama ya chini kwenye kuna ukosefu wa msaada wa kijamii.

→ Muundo wa serikali kujenga uratibishaji na ushirikiano

Jambo ambalo halipewi uzito ni umuhimu wa kuwa na mfumo rasmi serikalini unaowalenga wanawake katika mfumo wa mahakama za jinai. Bila kutambua hili katika idara mbalimbali na wizara, vifungu vinavyohusu jinsia vikwazo vya kifungo cha nje havitakuwa na uthabiti piavitapuuzwa.

Kwa kuanza, serikali lazima ianzishe sera kuu ya taifa inayotilia mkazo sheria za Bangkok ilikuwe na mwelekeo wa kuzingatia jinsia katika mfumo wa mpangilio ya kuendesha kesi za uhalifu. Pia ni muhimu na chombo uratibishaji ambacho kinaweza kuwakutanisha wadau wanaohusika ili kubadilishana taarifa namna wanavowatendea wanawake watuhumiwa na wahalifu. Kuongeza mashirikiano kunaweza kusaidia kuimarisha utoaji wa msaada wa ziada kwenye miradi inayohusu wanawake wanaotumikia vikwazo kwa jamii kwa kuwashirikisha wasimamizi wa miradi inayoshughulikia maswala ya afya ya akili, madawa ya kulevya na pombe.

> "Ijaapokuwa tulifanya kazi kwa bidii na watumishi wa uma, tulifanya kazi na watumishi wa serikali, na muitikio wa wakati huo ulikuwa, "Idadi ya wanawake ilikuwa 5% tu ya jumla ya wafungwa." Yalikuwa mapambano makubwa kuweza kusikilizwa. Mabadiliko ambayo yaliunganisha kazi zote za idara yaliifanya timu kuwa kubwa mno."

Maswali Bungeni, United Kingdom.[13]

Machapisho zaidi

Taarifa kamili ya utafiti

Huduma kwa Jamii na Amri ya Majaribio kwa wanawake: utafiti nchini Kenya

Inapatikana mtandaoni: www.penalreform.org/resource/community-service-and-probation-for-women-a-study/



Makala fupi

Haki sawa: Kuleta mafankio kwenye mpango wa Vikwazo kwa jamiinchini Kenya

Ainisha manufaa na changamoto zinzowapata wanawake wanaotumikia vikwazo kwa jamii. Habari kutokana na mahojiano na wanawake wahalifu nchin Kenya, Majaribio na Huduma ya ufuatiliaji baada ya kuwa Probation and Aftercare Service and Penal Reform International.

Dakika 7. Inapatikana mtandaoni: www.penalreform.org/resource/equal-justice-making-community-sanctions-work-women-kenya/

Zana za kufanyia kazi on UN Bangkok Rules

Mkusanyiko wa machapisho ya kusaidia kuweka kwenye utekelezaji Sheria za UN. Hizi ni pamoja na Nyaraka ya muongozo, Kielelezocha utekelezaji na mafunzo ya bure kwa njia ya mtandaoni.

Inapatikana mtandaoni: www.penalreform.org/priorities/women-in-the-criminal-justice-system/bangkok-rules-2/tools-resources/





References

1. Gender-sensitive (or gender-responsive) practices are 'practices, programs, assessments, or policies that account for the differences in characteristics and life experiences that women and men bring to the justice system and that have been tested by methodologically rigorous research and found to be effective in reducing recidivism'. (National Resource Center on Justice Involved Women, *Gender Responsive Interventions in the Era of Evidence-Based Practice: A Consumer's Guide to Understanding Research*, p1.)
2. Kwenye utafiti huu, walihojiwa wanawake wahalifu 97 nchini Kenya walihojiwa ambao walikuwa wanatumikia au walikuwa wametumikia Amri ya mahakama ya kufanya huduma za jamii au amri ya kifungo cha nje na wamewahi kuishi katika mikoa mbalimbali, pia walihojiwa wanawake waliokuwa kwenye kifungo cha ndani ya hosteli. Maafisa 22 wa mahakama, Maafisa 22 wa vifungo vya njena wasimamizi 18 wa huduma za jamii na wadau wengine muhimu walihojiwa. Utafiti huu ulifanyika kati ya mwezi Februari na Aprili 2016 kwenye maeneo tofauti nchini. Kwa maelezo zaidi kuhusu methodojia, angalia taarifa kamilia ambayo inapatikana kwenye tovutit: www.penalreform.org/resource/community-service-and-probation-for-women-a-study/ <taarifa ilipatikana tarehe tarehe 13 Oktoba 2016>.
3. Soma Penal Reform International's research series, *Who are women prisoners?*, ambacho kinajumuisha taarifa nne ambazo zinatoa taswira za undani wa wanawake walio magerezani katika nchi nne katika mikoa minne, taarifa zinapatikana: www.penalreform.org/priorities/women-in-the-criminal-justice-system/bangkok-rules-2/research <taarifa ilipatikana tarehe 20 Oktoba 2016>. Soma pia, Penal Reform International/Andrea Huber, *Women in criminal justice systems: the added value of the UN Bangkok Rules*, 2015.
4. 'Wahalifu wadogo kuachiwa huru kwa lengo la kupunguza msongamano Kenya prisons', *The Standard Kenya*, 4 October 2016, www.standardmedia.co.ke/article/2000218320/petty-offenders-to-be-released-in-bid-to-decongest-kenya-prisons <Utathmini ulifanyika 13th October 2016>.
5. The Kenya Demographic and Health Survey of 2014 found that more than one third of ever-married women reported that they had experienced physical violence by their husband or partner; 32% reported emotional violence, and 13% reported sexual violence; almost half (45%) of women aged 15-49 had experienced physical violence. Available at: www.dhsprogram.com/pubs/pdf/SR227/SR227.pdf <accessed 21 September 2016>.
6. Tokyo Rules, Rule 7.1
7. In Kenya, Probation Orders involve regular meetings with a probation officer to discuss progress. Supervision plans are geared towards rehabilitation and may include counselling, or restorative processes such as mediation, where these services are available. Probation officers supervising a woman offender should be female although this is not always observed in practice.
8. In Kenya, Community Service Orders require an offender to engage in unpaid public work for the benefit of the community for a specified period.
9. In Uganda, the Community Service Department found that mixing up different stakeholders in one training session helped pave the way for a better understanding of community service issues and ideas on how to move forward together. See Penal Reform International, *Excellence in Training on Rehabilitation in Africa (ExTRA) Project, mid-term evaluation*, January 2016, p40.
10. Kwa maelezo zaidi, angalia Penal Reform International, *Excellence in Training on Rehabilitation in Africa (ExTRA) Project: Community Service as an Alternative to Imprisonment, final evaluation*, Septemba 2016.
11. See for example, UN Women, 'Virtual knowledge centre to end violence against women and girls, Consequences on individuals and communities', available at: www.endvawnow.org/en/articles/1476-consequences-on-individuals-and-communities.html <accessed 27 October 2016>.
12. Rule 60 of the Bangkok Rules promotes interventions alongside the application of non-custodial alternatives for women offenders, which should take account of the 'need to provide care for children and women-only services'.
13. Extract from *The Corston Report: A report by Baroness Jean Corston of a review of women with particular vulnerabilities in the criminal justice system*, Home Office, UK, March 2007.

Penal Reform International (PRI) *Mageuzi Adhabu Kimataifa* ni shirika lisilo la serikali ambalo ambalo linaendeleza na kukuza usawa, ufanisi na majibu yenye uwiano kwenye matatizo ya mahaka za jinai duniani kote.

Tunasimamia uanzishaji wa mbadala wa magereza kusaidia marekebisho kwa wahalifu na tunaanzishana kutetea haki za wafungwa kutendewa usawa na kiutu. Tunafanya kampeni za kuzuia mateso na kupinga adhabu za kifo, na tunajitahidi kuhakikisha watoto na wanawake wanapata majibu yanayostahili kwa haki wanapokutana na sheria.

Kwa sasa tuna programu Mashariki ya kati na Kaskazini mwa Afrika, Maeneo ya Jangwa la Sahara Afrika (Sub Saharan Africa), Mashariki mwa Ulaya (Eastern Europe), Katikati ya Asia (Central Asia) na Kusini mwa Caucasus (South Caucasus), pia tunafanya kazi na washirika Kusini mwa Asia (South Asia).

Ukihitaji kupokea Toleo la gazeti letu kwa mtandaoe newsletter, Jisajili kwenye tovuti: www.penalreform.org/keep-informed.

Kenyan Probation and Aftercare Service ni msimamizi pekee wa vikwazo nchini Kenya.

Idara hii ni moja ya wakala ambao wanaunda mfumo wa mahakama ya Jinai Kenya na inawajibika kutekeleza usimamizi wa kifungo cha nje na huduma za kurekebisha tabia ndani ya jamii. Tunasukumwa na nia ya kuleta mageuzi na kusababisha mabadiliko chanya kwenye maisha ya wahalifu. Tunaamini kwamba wahalifu wanaweza kubadilika wakipewa nafasi nyingine kwa kutoa marekebisho na kuwatendea inavyostahili.

Chapisho hili limetolewa chini ya mradi ambao umefadhiriwa the Thailand Institute of Justice.

Chapisho linaweza kufanyiwa marekebisho, kuchapishwa upya, kutafsiriwa, kwa sehemu au lote lakini haliruhusiwi kuliuza kwa malengo ya kibiashara. Mabadiliko yoyote maandiko yaliyomo lazima yaidhinishwe na Penal Reform International. Pia unatakiwa kwenye nukuu kutambua haki miliki za shirika Penal Reform International kwenye chapisho hili.

Email: publications@penalreform.org
© Penal Reform International 2017

Penal Reform International
1 Ardleigh Road
London N1 4HS
United Kingdom

+44 (0) 207 923 0946
www.penalreform.org
Twitter: @PenalReformInt

Kenya Probation and Aftercare Service
Taifa Road, Reinsurance Plaza, 11th Floor
P.O. Box 42335-00100 GPO
Nairobi
Kenya

www.probation.go.ke

Funded by

TIJ
THAILAND INSTITUTE OF JUSTICE